

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HWK/L.2/II/VOL.VII/44

Tarehe: 21/07/2023

Mkurugenzi Mtendaji,  
Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC)  
S.L.P 938,  
**DAR ES SALAAM**

**KUH: MAOMBI YA UTHIBITISHO WA UMILIKI WA ENEO LENYE UKUBWA WA HEKTA 10 LILILOPO CHEKELEI HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE.**

Tafadhali Husika na somo tajwa hapo juu.

2. Nakiri kupokea barua yenye Kumb.Na. CA.148/234.01.D/141 ya tarehe 08 Juni, 2023 iliyohusu mada tajwa hapo juu.
3. Katika barua yanu mmeleza kuwa ardhi husika ilipatikana baada ya kampuni **Dazhanhongt Co. Limited** kuinunua kutoka kwa **Bi. Mwajuma Hassan Shengombe** mkazi wa kijiji cha Chekelei.
4. Napenda kukufahamisha kwamba, baada ya kufanya uchunguzi wa kina hadi ngazi ya kijiji husika tumebaini kutokuwepo kwa taarifa za mauziano hayo baina ya kampuni ya **Dazhanhongt Co. Limited** na **Bi. Mwajuma Hassan Shengombe**.
5. Hata hivyo imethibitika kwamba **Bi. Mwajuma Hassan Shengombe** hamiliki ardhi yenye ukubwa huo hapo kijijini.
6. Hivyo basi, kutokana na maelezo hayo hapo juu halmashauri ya wilaya ya Korogwe imeshindwa kuthibitisha umiliki wa eneo hilo kwa kampuni ya **Dazhanhongt Co. Limited**.
7. Nakutakia kazi njema.

Halfan H. Magani  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**



**Nakala:** Mkurugenzi,  
Dazhanhongt Co. Limited,  
S.L.P 32975  
**DAR ES SALAAM.**

- Kwa taarifa